

KIKAO CHA PILI CHA MTA A WA KILOMBERO 2026

April 19, 2026 sunday

Wajumbe

- | | |
|--------------------------|------------|
| 1. Mumbara Peter Mumbara | Mwenyekiti |
| 2. Upendo john | Katibu |
| 3. Frank joseph | Mjumbe |
| 4. Peter magoti | Mjumbe |
| 5. Simon kinyonyi | Mjumbe |
| | |
| 5. Wema mbwambo | Mjumbe |
| 6. Naftal mbwambo | Mjumbe |
| 7. Grace obadia | Mjumbe |
| 8. Grace bigambo | Mjumbe |
| 9. Godwin kabogo | Mjumbe |
| 10. Alphaxade joshua | Mjumbe |

AGENDA

- 1.Kufungua kikao
- 2.Atape Day
- 3.Nyumba Nyamvisi
- 4.Vitabu vya Makambi
- 5.Njombe net event
- 6.Masomo ya majuma ya maombi na kubadilishana wahudumu
- 7.Nyumba ya mchungaji
- 8.Efoti ya mtaa
- 9.Matoleo ya zaka na sadaka
- 10.Sadaka ya mazao
- 11.Jukwaa la mtaa
- 12.Kalenda ya matukio
- 13.Kiongozi wa A.M.R wa mtaa
- 14.Semina ya Wazee
- 15.Kufunga kikao

1.Kufungua kikao

- Kikao kilifunguliwa mnamo saa 9:30 alasiri chini ya usimamizi wa mchungaji wa mtaa mumbara na ombi la ufunguzi kutoka kwa peter magoti.

2.Atape Day (semina za ujasiriamali)

- Kutakua na semina za ujasiriamali zitakazo fanyika mtaa wa

kilombero, wajumbe walipendekeza kuwa semina hiyo itafanyika mwisho ni mwa wiki la mwisho wa mwezi wa tisa. Pia litafanyikia katika kanisa la mkamba katika siku ya jumamosi mchana na jumapili. Gharama ya malazi na usafiri ni juu yao mtaa utawahudumia kwa chakula tu waendesha semina.

3.Nyumba ya nyamvisi

- Kuhusu ununuzi wa nyumba ya nyamvisi inayotakiwa kununuliwa, wajumbe walikubaliana kuwa kila kanisa lione namna ya kuwasaidia mchango wa ununuzi wa nyumba ya nyamvisi kila kanisa watoe kulingana na vile walivyo barikiwa.

4.Vitabu vya Makambi

- Wajumbe walikubaliana kununua kuanza vitabu vya makambi kwa kila kanisa kulingana na idadi ya washiriki wao walio makanisani.

5.Njombe net event

- Katika mahubiri ya satellite ya njombe net event tathimini ya vituo vya makanisa vitakao oneshwa kutoka katika makanisa yetu, nikama ifuatavyo;

(i)MKAMBA KITUO 1

(ii)NYAMVISI VITUO 2

(iii)KIDATU KITUO 1

(iv)KILOMBERO 1

6.MASOMO YA MAJUMA YA MAOMBI NA KUBADILISHANA WAHUDUMU

- ★ Maadhimio ya kuhusu masomo ya juma la maombi taarifa ni kwamba uongozi wa kanisa uwe unakusanya pesa kwa washiriki na kuzituma kwaajili ya kununulia vitabu vya kujifunzia katika juma la maombi kabla ya masomo kuanza ili kila mshiriki wawenavyo wakati wa masomo yanaendesha.
- ★ Kuhusu kubadilishana wahudumu kutoka kanisa moja kwenda katika kanisa lengine wakiwa wanaitaji huduma ya mhudumu yeyote katika kanisa lengine kanisa linalo itaji huduma ya mtumishi huyo linapasa kushiliki kutoa gharama zote za nauli kumsafirisha mhudumu.

7.Nyumba ya mchungaji

- Kuhusu nyumba ya mchungaji wajumbe walikubaliana

kuwa kutaundwa kamati ya kufanya tathimini ya gharama zote kuanzia kununua kiwanja hadi ujenzi wa nyumba kukamilika. Kisha kila kanisa litapangiwa kiasi cha kuchangia na mpango huu utachukua miaka mitano na utekelezaji wake utanza kuanzia mwakani 2027.

- Wanakamati waliopendekezwa ni wakuu wa majengo wote wa mwaka huu 2026 wa makanisa yote, ambao ni wafuatao;
- NYAMVISI - FREDI FELIX
- MKAMBA - HAPPINESS SAGWA
- KIDATU - JULIUS MASHAURI
- KILOMBERO - ALOIS SULE
- KIDODI - GEORGE MDESA
- KITETE -

8.Efoti ya Mtaa

- Wajumbe walikubaliana efoti ya mtaa utekelezaji wake ufanyike mwakani 2027.

9.Matoleo ya zaka na sadaka

- Mapendekezo ya wajumbe ni kuwa kila mkuu wa uwakili awe anatoa semina kwa washiriki pamoja na taarifa ya utoaji wake wa zaka na sadaka.

10.Sadaka ya mazao

- Wajumbe wamekubaliana kuwa kila mshiriki awe anatoa sadaka ya mazao,
- **Mfano**; mpunga,, mahindi, yani kile ambacho mtu atachokuwa amelima ndicho akitoe.

11.Jukwaa la mtaa

Matengenezo ya jukwaa yamekamilika na jukwaa limeshawaliwa, hivyo gharama yamatengenezo imetumika kama ilivyopigiwa hesabu hapo awali 420,000/=

12.Kalenda ya matukio

Kalenda ya matukio zilikuja tatu hivyo zimegawiwa kwenye makanisa matatu ambayo ni MKAMBA, KIDATU, NA NYAMVISI.

13.Kiongozi wa A.M.R wa mtaa

Kiongozi wa mtaa wa AMR aliyependekezwa ni ndugu
FILEMONI NGOGO.

14.Semina ya wazee wa makanisa.

Makanisa ambayo yatakayo hudhuria semina ya wazee ni
makanisa matatu, hivyo wazee watakao hudhuria semina
hiyo ni watatu kwa kila kanisa ataenda mzee mmoja.

15.Kufunga kikao

Kikao kilifungwa mnamo saa 11:32 jioni na ombi la
kufunga kikao lilitolewa na EDISONI KANYIKA.
